

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
22 Desemba 2007**

Waliohudhuria

Ally Saidi Mwishehe

Ally Salum

Aseli Wilison

Elaine Baker

Filbert Mbecha

Husein Hamza Hamisi

Juma Ali Salehe Jongo

Jumanne Idd Selemani

Kassim Bakari

Paulo Atibu Hatibu

Yusufu Juma

Ofisi

Elaine alileta dondoo za mkutano kutoka januari 2006 mpaka oktoba 2007 ambazo zimetafsiriwa kwa kiswahili. Dondoo zitabaki kwenye rafu za ofisi ili wanachama wanaweza kuzisoma kwa muda wao. Atajaribu kuandika dondoo zinazobaki kwa kiswahili mwenyewe.

Ubao wa matangazo bado wanatengenezwa.

Guta

Wakati wa wiki Juma na Elaine walitoa Tsh 60,000 kutoka benki na Juma alikuwa akibaki na Tsh 40,000 ya hela ya UWABA, na Juma na Jumanne walitumia hela hiyo Tsh 100,000 kununua mipira mpya kwa ajili ya guta (Tsh 50,000), kasi mpya (Tsh 20,000) na bao (Tsh 30,000). Juma ana risiti kwa mipira na kasi na Jumanne atapata risiti kwa bao.

Mambo ya hela

Elaine ataleta kadi ya kushukuru wiki ijayo ambayo wanachama watasaini kuwashukuru Bike Nouveau Fabriq, Italia.

Ubalozi wa Uholonzi waliona kosa na walirekebisha kwa kutupa hundi nyingine kwa Tsh 230,700 ambayo iliwekwa benki wakati wa wiki.

Mejah alisema kwenye simu atashughulika kutengeneza T-shirt na kununua helmeti kwa wanachama.

Chuo cha Usafirishaji (NIT)

Elaine aliongea na Bwana Wemba kwa simu na walikubali tarehe 19 januari 2008 iwe tarehe ya semina ya usalama barabani kwa wapanda baisikeli huku Chuo cha Usafirishaji. Wanachama wote kwenye mkutano walisema watahudhuria.

Halmashari ya Jiji na TANROADS

Bado hatujapata majibu ya barua tulizotumia halmashari ya jiji kuhusu Mpango Madhubuti wa Usafiri Dar es Salaam. Pia bado hatujapata jibu kutoka TANROADS.

Posho kwa Juma

Kwa sababu Juma anafanya kazi ya ufuataliaji ya kila siku ya UWABA zaidi ya mtu mwingine, na mara nyingi anaendesha baisikeli jiji nzima kutoa na kufuatalia barua, Elaine alipendekeza kwamba alipwe posho ya hiyo kazi. Alipendekeza kiasi ndogo ya Tsh 20,000 kwa mwezi mpaka hela inatosha kulipa zaidi. Mpaka sasa amefanya kazi hiyo kwa miaka miwili kwa kujitolea bila malipo, na mara nyingi anafunga duka lake wakati wa kufanya kazi za UWABA. Wanachama wengine walikubali kwamba inafaa kumlipa Juma hiyo posho kila mwezi.

Polisi wa trafiki na sheria za barabara

Paulo alipendekeza kwamba tukutane na polisi wa trafiki. Ilikubalikwa kwamba tuongee nao kuhusu sheria za barabara na vipi zinahusika na wapanda baisikeli, mambo ya utekelezaji wa sheria kulinda wapanda baisikeli, na vipi wanachama wa UWABA wanaweza kuwasaidia polisi wa trafiki kwa kutoa repoti.

Tulikubali kwamba ni muhimu wanachama wajue sheria za barabara. Elaine alisema ataprintia Road Traffic Act (ambayo ni kwa kiingereza), lakini haina pointi nyingi kuhusu wapanda baisikeli na inaonekana pointi nyingi zaidi zipo kwenye sheria ndogo (regulations) zinasainiwa na Waziri na sheria ndogo zinazopitiwa na halmashari za serikali za mitaa. Paulo alisema atawaomba HUWATA kutupa nakala za hizi sheria kama wanazo, na Elaine pia atajaribu kupata nakala kutoka shirika za kisheria au kwenye intaneti.

Mengineo

Filbert alipendekeza kwamba kama wanachama wanasaini kurasa ya mahudhurio basi wabaki kwa mkutano mzima mpaka ajenda inamaliza.